JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA A (GATCE) 2021

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA A (GATCE) 2021

## 621 KISWAHILI

*Imechapwa na*:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021.**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ........ 2

2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Fasihi Simulizi ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Stadi za Lugha ........ 4
2.1.3 Swali la 3: Sarufi ........ 7
2.1.4 Swali la 4: Ufahamu ........ 10
2.1.5 Swali la 5: Fasihi Simulizi ........ 13
2.1.6 Swali la 6: Mbinu za Kufundishia na Kujifunza Kiswahili ........ 16
2.1.7 Swali la 7: Utungaji ........ 18
2.1.8 Swali la 8: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili ........ 20
2.1.9 Swali la 9: Ufahamu ........ 23
2.1.10 Swali la 10: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ........ 26
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha ........ 29
2.2.1 Swali la 11: Fasihi Simulizi ........ 30
2.2.2 Swali la 12: Stadi za Lugha ........ 34
2.2.3 Swali la 13: Utungaji ........ 37
2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha ........ 42
2.3.1 Swali la 14: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ........ 42
2.3.2 Swali la 15: Upimaji ........ 46
2.3.3 Swali la 16: Mbinu za Kufundishia na Kujifunza Kiswahili ........ 50

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA ........ 56

4.0 HITIMISHO ........ 57

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 57

Kiambatisho A ........ 59

Kiambatisho B ........ 60

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu Ualimu Daraja la A 2021 kwa somo la Kiswahili imeandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania ili kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa kwa wakaguzi, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla. Matokeo ya watahiniwa katika mtihani huu ni kipimo kinachoonesha jinsi mchakato mzima wa elimu ulivyofanikiwa kuwapa elimu walimu tarajali kupitia wakufunzi wao.

Taarifa inaonesha namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali kwa kutumia maarifa waliyopata. Uchambuzi unaonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2021 ni mzuri kwani asilimia 99.94 ya watahiniwa walifaulu. Sababu mbalimbali zilizochangia watahiniwa kufaulu vizuri mtihani huu katika baadhi ya mada zimeainishwa kuwa ni pamoja na: uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa, matumizi sahihi ya lugha na alama zote za uandishi, uzingatiaji wa matakwa ya swali na kutoa hoja sahihi zenye mifano thabiti. Vile vile, sababu mbalimbali za watahiniwa kupata ufaulu wa wastani zimeoneshwa ikiwa ni pamoja na kutoa majibu yasiyojitosheleza na kutokuwa na stadi za kutosha za uandishi wa majibu ya insha.

Vile vile, sababu za watahiniwa kuwa na kiwango hafifu cha ufaulu zimeainishwa ikiwa ni pamoja na kukosa mtiririko mzuri katika majibu yao, kutoandika utangulizi na hitimisho katika maswali ya insha na kukosa weledi wa dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa Taarifa hii itatoa mrejesho utakaowawezesha wakuu wa vyuo, wakufunzi na wanachuo kutumia mbinu muafaka katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika vyuo vya ualimu.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linawashukuru wakufunzi, maafisa mitihani na wadau wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Charles Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inaonesha uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Ualimu Daraja la A kwa somo la Kiswahili uliofanyika Mei, 2021. Mtihani huu ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyogawanyika katika sehemu A, B na C ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne (14). Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi, mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote ambapo kila swali lilikuwa na alama nne (4) na kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 40. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) ya insha kutoka katika mada za taaluma. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili ambapo kila swali lilikuwa na alama 15 na kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 30. Sehemu C ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) ya insha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali (2) yenye alama 15 na kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 30.

Jumla ya watahiniwa 3,262 waliosajiliwa kufanya somo la Kiswahili walifanya mtihani wa Ualimu daraja A katika somo la Kiswahili. Kati yao wasichana walikuwa 1,503 na wavulana walikuwa 1,759. Kiwango cha ufaulu katika somo hili kilikuwa kizuri kwani asilimia 99.94 ya watahiniwa walifaulu. Kiwango hiki cha ufaulu kwa mwaka 2021 kimepanda kwa asilimia 0.03 ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo walifaulu kwa kiwango cha asilimia 99.91. Pamoja na ufaulu mzuri wa jumla, watahiniwa wachache walipata ufaulu wa wastani na hafifu katika baadhi ya maswali.

Uchambuzi huu umegawanyika katika madaraja matatu ambayo ni: ufaulu mzuri unaoanzia asilimia 70 mpaka 100, ufaulu wa wastani unaoanzia asilimia 40 mpaka 69 na ufaulu hafifu unaoanzia asilimia 0 mpaka 39. Aidha, chati za viwango vya ufaulu kiasilimia zimetumika kwa kila swali ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Taarifa hii pia imechambua jinsi watahiniwa walivyojibu katika kila swali. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa kama vielelezo vya majibu halisi ya watahiniwa. Aidha, tathimini ya ufaulu kwa mada, hitimisho na mapendekezo vimewasilishwa pia.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Uchambuzi wa takwimu kwa kila swali umefanyika ambapo ufaulu kwa watahiniwa umegawanyika katika makundi matatu ambayo ni ufaulu wa kiwango kizuri, kiwango cha wastani na kiwango hafifu. Mtahiniwa aliyepata kiwango kizuri cha ufaulu alipata alama kuanzia 3 hadi 4, kiwango cha wastani cha ufaulu alipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na kiwango hafifu cha ufaulu alipata kuanzia alama 0 hadi 1.5.

## 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali kumi (10) yaliyohitaji majibu mafupi ambayo yalitungwa kutoka katika mada za Taaluma na Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali yote ambapo kila swali lilikuwa na uzito wa alama nne (4) na kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 40.

### 2.1.1 Swali la 1: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi Simulizi na lilimtaka mtahiniwa aeleze kwa kifupi tanzu nne za Fasihi Simulizi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3,261. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani watahiniwa 2,491 sawa na asilimia 76.4 walipata alama za wastani na zaidi. Swali lilikuwa katika ngazi ya kukumbuka. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali la 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 991 sawa na asilimia 30.4 walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada hii. Watahiniwa hawa waliweza kueleza kwa kifupi tanzu nne za fasihi simulizi huku wakitoa mifano na wengine waliweza kujibu swali kwa usahihi kabisa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua tanzu hizo kwa kutoa mifano ambapo alieleza kuwa, *Hadithi ni masimulizi yenye lugha ya nathari ambayo huwa na mtiririko wa matukio unaokamilisha kisa mfano visakale na soga. Ushairi ni utanzu wa fasihi simulizi wenye kutumia lugha za mkato na maneno yaliyopangiliwa vizuri katika ubeti kwa hali ya kuimbika mfano nyimbo na tenzi. Semi ni utanzu wa fasihi simulizi ambao hutumia lugha ya picha na mafumbo yaliyofichika yenye kuueleza ukweli wa maisha mfano methali, nahau na Sanaa za maonesho ni ufundi wa kuwasilisha mawazo yaliyopo katika fikra za binadamu katika hali ya utendaji mfano majigambo na tambiko.* Kielelezo Na. 1.1 ni miongoni mwa sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa.


1. Tanzu za fasihi simulizi ni:-
i) Hadithi; ni tanzu ya fasihi simulizi ambayo hutumia lugha ya nasari katika masimulizi. vipera vyake ni soga, Vigano tarihi, na ngano.
ii) Sanaa za maonesho; ni tanzu ya fasihi simulizi ambayo huhusika na maonesho ya jukwaani vipera vyake ni majigambo, ngonjera, mivinga, uchoraji, uhumi.
iii) Ushairi; ni tanzu ya fasihi simulizi ambayo huwa katika mfumo wa beti katika uwasilishaji wake vipera vyake ni shairi, Tenzi, nyimbo, ngonjera.
iv) Semi; Ni tanzu ya fasihi simulizi ambayo huwa katika mafumbo yana yohitaji kufumbuliwa vipera vyake ni Nahau, methali, vitendawili.

**Kielelezo Na. 1.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 1

Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza tanzu nne za fasihi simulizi kwa kutoa mifano thabiti.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 1,500 ambao ni sawa na asilimia 46 walipata alama za wastani kati ya 2 na 2.5 kutokana na kuandika baadhi ya tanzu za Fasihi simulizi na kushindwa kutoa maelezo ya kufafanua tanzu hizo, wengine walishindwa kuelewa tofauti kati ya tanzu za fasihi simulizi na vipera vya fasihi simulizi hivyo walichanganya dhana hizo na wachache walitaja tu tanzu za Fasihi Simulizi bila kuzitolea maelezo. Hivyo, walipata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja na alitaja tanzu sahihi za fasihi simulizi kuwa ni *methali na semi.* Pia, alitaja zisizo sahihi kama vile*; ufinyanzi, uchoraji, ngonjera* na *muziki.*

Hata hivyo, watahiniwa 770 sawa na asilimia 23.6 walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo, badala ya kueleza tanzu za fasihi simulizi, walielezea kazi na vipera vya fasihi simulizi, wengine walielezea wahusika wa fasihi simulizi kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza aina za hadithi kama vile; *vigano, ngano, soga* na *tarihi* badala ya tanzu za fasihi simulizi. Majibu haya yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya tanzu za fasihi simulizi. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.



| | | |
|---|---|---|
| 1. | i/ Kuburudisha jamii | |
| | ii/ Kuelimisha jamii | |
| | iii/ Kufurahisha jamii | |
| | iv/ Kurahisha Mawasiliano | |

**Kielelezo Na. 1.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 1

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kazi za fasihi simulizi badala ya kutaja na kueleza tanzu za fasihi simulizi baada ya kushindwa kuelewa matakwa ya swali.

### 2.1.2 Swali la 2: Stadi za Lugha

Swali hili lilitoka katika mada ya Stadi za Lugha na lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi jinsi stadi za kuandika na kuzungumza zinavyotofautiana katika vipengele vya (a) Kiwakilishi (b) Kikomo

(c) Uhusiano na (d) Suluhisho. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote 3,262 (100%) waliofanya mtihani huu.

Swali hili lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya ambapo watahiniwa 2,810 sawa na asilimia 86.1 walipata alama hafifu. Chati Na. 2 inafafanua viwango vya ufaulu katika swali la 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama hafifu walikosa maarifa juu ya stadi za kusoma na kuzungumza kwani badala ya kueleza tofauti kati ya stadi ya kuandika na kuzungumza katika vipengele vya kiwakilishi, kikomo, uhusiano na suluhisho, walieleza dhana za vipengele hivyo. Hata hivyo, wengine walieleza kazi za kiwakilishi katika sentensi na wengine walieleza dhana ya uhusiano kuwa ni *tendo la kuwa wapenzi*. Vile vile, wapo walioeleza kuwa *kikomo ni mwisho wa jambo* na suluhisho ni *kufanya upatanisho kwa watu waliogombana* jambo linaloashiria kwamba watahiniwa hawa walikosa maarifa pamoja na kushindwa kubaini matakwa ya swali. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.



2. (a) Kiwakilishi - ni neno linalokaa badala
ya nomino. Mfano "Yule ni
mfupi sana"

(b) Kikomo - ni kitu cha mwisho katika sente
nsi. Mfano " Mimi nacheza mpira".

(c) Uhusiano - ni muunganiko wa vitu viwili au
zaidi. Mfano uhusiano wa kifami-
lia baba, mama na ndugu.

(d) Suluhisho - ni maamuzi ya mwisho katika
jambo fulani. Mfano " Mwizi
amekamatwa" Uamuzi wa mwi-
sho auawe.

**Kielelezo Na. 2.1**: Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 2

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa maana za maneno bila kuzingatia stadi za kuandika na kuzungumza.

Kadhalika, watahiniwa 371 sawa na asilimia 11.4 walipata alama za wastani ambapo, waliweza kueleza kwa usahihi baadhi ya tofauti zilizopo katika vipengele vya stadi ya kuandika na kuzungumza na walishindwa katika vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi tofauti iliyopo kati ya stadi hizo katika kipengele cha *Kikomo* kuwa kwa mzungumzaji ni *kusikiliza* na katika kuandika ni *kusoma*. Aidha, katika kipengele cha *uhusiano* mzungumzaji na msikilizaji *huwa karibu sana*, yaani ana kwa ana na kimaandishi mwandishi na msomaji *huwa mbali*. Lakini alishindwa kuelezea vipengele vingine. Hivyo, alipata alama za wastani.

Watahiniwa 81 (2.5%) waliweza kujibu swali hili vizuri kwani waliweza kupitia vipengele vya kiwakilishi, kikomo, uhusiano na suluhisho. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.



2 (a) Kiwakilishi
Stadi ya kuandika huwakilishwa kwa njia ya maandishi lakini stadi ya kuzungumza huwakilishwa kwa njia ya mazungumzo au kuongea.

(b) Kikomo
Stadi ya kuandika kikomo chake ni kwa wanaojua kusoma na kuandika lakini stadi ya mazungumzo kikomo ni ya jamii zima.

(c) Uhusiano
Stadi ya kuandika haikutanishi au haihusianishi fanani na hadhira lakini stadi ya mazungumzo hukutanisha fanani na hadhira.

(d) Suluhisho
Stadi ya kuandika mwandikaji pekeake ndiye hubaini suluhisho la matatizo pindi yanapojitokeza lakini stadi ya mazungumzo msikilizaji na mzungumzaji hubaini suluhisho la tatizo pindi linatokea

**Kielelezo Na. 2.2**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2

Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja tofauti zilizopo kati ya stadi ya kuandika na kuzungumza kutokana na kuelewa matakwa ya swali pamoja na kuwa na maarifa ya kutosha.

### 2.1.3 Swali la 3: Sarufi

Swali lilitoka katika mada ya Stadi za Lugha na lilikuwa mahsusi kupima maarifa. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote 3,262. Swali

lilimtaka mtahiniwa kuandika sentensi alizopewa katika kauli ya kutenda. Watahiniwa 2,530 sawa na asilimia 77.6 walipata alama za nzuri kuanzia 2 hadi 4. Chati Na. 3 inafafanua viwango vya ufaulu katika swali la 3.




**Chati Na. 3 :** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Uchambuzi katika chati Na.3 unaonesha kuwa watahiniwa 2,261 sawa na asilimia 69.3 walifaulu kwa kupata alama 3 hadi 4 kutokana na sababu zifuatazo: Baadhi ya watahiniwa waliweza kuandika kwa usahihi sentensi nyingi na kushindwa kuandikia sentensi chache lakini wengine waliweza kuandika kwa usahihi sentensi zote nane walizopewa katika kauli ya kutenda. Majibu ya watahiniwa hawa yanaonesha kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya matumizi ya kauli za utendaji. Kielelezo Na 3.1 ni moja ya sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.



3. (a) Mtoto amecheza mpira
(b) Fundi amemaliza kazi
(c) Askari amewapiga wezi
(d) Mimi nimekausha nguo.
(e) Mama amewapiga watoto wake.
(f) Mfungaji ameingiza vizuri mpira.
(g) Mbwa wa Jirani amemla Kuku wa baba.
(h) Rafiki yake Juma amemuita.

**Kielelezo Na. 3.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 3

Kielelezo Na. 3.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika kwa usahihi sentensi katika kauli za kutenda.

Watahiniwa 269 sawa na asilimia 8.3 walifaulu kwa kupata alama kuanzia 2 na 2.5. Watahiniwa hao waliweza kuandika kwa usahihi baadhi ya sentensi katika kauli ya kutenda na kushindwa katika sentensi nyingine. Aidha, wengine waliandika kwa usahihi kauli ya utendaji lakini wakashindwa kuandika nyakati sahihi katika sentensi hiyo. Aidha, baadhi ya watahiniwa waliweza kuandika kauli ya kutenda lakini wakashindwa kuandika kwa usahihi upatanisho wa kisarufi kwa mtendwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;

*Mama <u>amepiga</u> watoto wake* badala ya *mama <u>amewapiga</u> watoto wake.*
*Mbwa wa jirani <u>amekula</u> kuku wa baba* badala ya *mbwa wa jirani <u>amemla</u> kuku wa baba.* Makosa hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya matumizi sahihi ya kauli ya kutenda katika lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, watahiniwa 732 sawa na asilimia 22.4 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa sababu walishindwa kuelewa matumizi sahihi ya kauli katika miktadha mbalimbali na kuandika kimakosa kauli walizopewa bila kuzingatia kauli za kutenda zilizotakiwa kwa mujibu wa matakwa ya swali. Watahiniwa wengine waliandika sentensi hizo katika kauli ya kutendewa na wengine waliandika kauli ya kutendwa badala ya kutenda. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika:

(a) *Mpira unachezwa na mtoto*
(b) *Kazi yote imemalizwa na fundi*
(c) *Wezi wamepigwa na askari*
(d) *Nguo zinakaushwa na mimi'*
(e) *Watoto wanapigwa na mama yao*
(f) *Mpira unaingizwa vizuri na mfugaji*
(g) *Kuku wa baba wanaliwa na mbwa*
(h) *Juma anaitwa na rafiki yake*

Kielelezo Na. 3.2 ni moja ya sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuandika sentensi katika kauli ya kutenda.


3 a) mpira umechezwa na mtoto
mpira unachezwa na mtoto
b) kazi yote imemalizwa na fundi
kazi yote inamalizwa na fundi
c) wezi wamepigwa na askari
wezi wanapigwa na askari
d) Nguo zimekaushwa na mimi
Nguo zinakaushwa na mimi
e) watoto wamepigwa na mama yao
watoto wanapigwa na mama yao
f) Mpira umeingizwa vizuri na mfungaji
mpira unaingizwa vizuri na mfungaji
g) Kuku wa baba ameliwa na mbwa wa jirani
kuku wa baba analiwa na mbwa wa jirani
h) Juma ameitwa na rafiki yake
Juma anaitwa na rafiki yake

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi Swali la 3

Kielelezo Na. 3.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeandika sentensi katika kauli ya kutendwa badala ya kauli ya kutenda.

### 2.1.4 Swali la 4: Ufahamu

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi dhana ya kusoma kwa ziada na kutaja hatua nne za kusoma kwa ziada. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 2,832 sawa na asilimia 87 ambapo watahiniwa

waliopata alama 2 hadi 4 ni 1,625 sawa na asilimia 63 kama inavyoonekana katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 1,281 sawa na asilimia 52.5 walikuwa na ufaulu wa wastani kwani walifaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao waliweza kutaja baadhi ya hatua za kusoma kwa ziada na kushindwa zingine. Baadhi yao walieleza dhana ya jumla ya kusoma kwa mfano, *Kusoma kwa ziada ni kitendo cha kutambua maandishi kwa lengo la kujipatia maarifa au habari.* Watahiniwa wengine waliweza kutaja hatua moja ya kusoma kwa ziada kati ya nne na wengine walitaja hatua mbili kati ya nne. Aidha, wengine walishindwa kutaja kwa usahihi hatua zingine za kusoma kwa ziada na kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja kwa usahihi hatua 2 za kusoma kwa ziada ambazo ni: *kubaini matini au vitabu* na *wanafunzi wasome matini au kitabu*.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 1,207 sawa na asilimia 37 ya waliojibu swali hili walipata kiwango hafifu cha ufaulu. Hii ilitokana na watahiniwa kutaja hatua ambazo sio za kusoma kwa ziada. Aidha, walishindwa kueleza dhana ya kusoma kwa ziada na hawakuweza kutaja hatua za kusoma kwa ziada. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kimakosa dhana ya kusoma kwa ziada kuwa ni: *Kusoma kwa sauti makala fulani au*

*matini na watu wengine wakisikiliza*. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali.


4(a) Kusoma kwa ziada,- Ni ile hali ya kusoma makala f
ulani au tarifa fulani kwa Sauti, amb
apo kuwa anasoma mtu mmoja kwa sauti
na wengine wanakuwa wanasikiliza

(b) Taja hatua nne za kusoma kwa ziada
(i) Kusoma kwa kufuata alama za uandishi
(ii) Msomaji awe anajiamini na awe anajua kusoma
(iii) Kuweka koma, nukta au ulizo pale inapostahi
(iv) Kusoma kwa kutoa Sauti

Kielelezo Na. 4.1**:** Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 4

Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja hatua za kusoma kwa ziada kwa sababu ya kukosa maarifa.

Watahiniwa 344 sawa na asilimia 10.5 walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa kuwa waliweza kueleza maana ya kusoma kwa ziada pamoja na kutaja kwa usahihi hatua nne za kusoma kwa ziada. Watahiniwa kutoka katika kundi hili walikuwa na maarifa ya kutosha pamoja na kuelewa matakwa ya swali.

Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.



04. (a) Kusoma kwa ziada ni aina mojawapo ya kusoma ambapo msomaji huweza kusoma kifungu cha habari kwa ajili ya kupata maarifa ya ziada juu ya kitu fulani. Mfano mtu kusoma gazeti kwa ajili ya Afya ya uzazi.

(b) Hatua za kusoma kwa ziada
- Chagua kifungu cha habari kutoka kwenye vitabu au magazeti.
- Anza kusoma kifungu hicho cha habari kwa usahihi na kuzingatia alama za uandishi.
- Chunguza mambo muhimu yaliyo katika kifungu hicho cha habari
- Chukua ujumbe au maarifa uliyoyapata kutoka kwenye habari hiyo

**Kielelezo Na. 4.2**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4

Katika kielelezo Na. 4.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza maana ya kusoma kwa ziada pamoja na kutaja hatua nne za kusoma kwa ziada.

### 2.1.5 Swali la 5: Fasihi Simulizi

Swali hili lilimtaka mtahiniwa aeleze maana ya dhana ya shairi, ngonjera, utenzi na kina kama zinavyotumika katika tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi. Swali lilijibiwa na watahiniwa wote 3,262. Watahiniwa 2,622 sawa na asilimia 80.4 walifaulu kwa kupata alama nzuri. Hivyo, kulifanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 5 inafafanua viwango vya ufaulu katika swali la 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 1,656 sawa na asilimia 50.8 walipata ufaulu wa wastani kwa kuwa waliweza kueleza baadhi tu ya maana ya dhana za kifasihi walizopewa kwa usahihi na kushindwa kueleza maana zingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi maana ya shairi kuwa ni *utungo wa kisanaa wenye mpangilio wa lugha ya mkato katika simulizi, maandishi au wimbo wenye mapigo ya kimuziki*. Aidha, alishindwa kueleza kwa usahihi maana ya ngonjera ambapo alieleza kuwa ngonjera ni *tungo inayotumia lugha ya maandishi ambayo huimbwa kufikisha ujumbe kwa hadhira.*

Halikadhalika, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 966 (29.6%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hawa waliweza kueleza maana ya dhana za kifasihi kwa kuzingatia matakwa ya swali kwani walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana za kifasihi. Kielelezo Na.5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu katika swali hili.


Q5: (a) Shairi - ni utungo wa kisanaa ambao hutumia lugha ya mkato, mvuto na yenye utaratibu maalumu wa mapigo ya kimuziki.

(b) Ngonjera - ni ushairi ulio katika mtindo wa majibizano baina ya watu wawili au zaidi na huwasilishwa kwa kuimbwa.

(c) Utenzi - ni masimulizi, mawaidha au maelezo marefu yanayotumia lugha ya mkato na huwa na mizani minane zaidi katika kila mstari, na vina vyake katika kila mstari hubadilika katika ubeti isipokuwa mstari wa mwisho ndiyo vina havibadiliki.

(d) Kina - ni silabi zinazojirudia mwishoni na katikati ya kila mshororo mmoja wa ubeti.

**Kielelezo Na. 5.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliweza kueleza dhana ya tanzu za fasihi simulizi kwa ufasaha na kupata alama za juu.

Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa, watahiniwa 640 sawa na asilimia 19.6 walifaulu kwa kiwango hafifu kwani walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao walishindwa kueleza maana ya shairi, ngonjera, utenzi na dhana ya kina, wengine walieleza kimakosa kuwa kina ni *sehemu ya ndani sana katika kazi ya fasihi*, shairi ni *utungo unaoonyesha mpangilio wa maneno*, sentensi, *uteuzi mzuri wa lugha ya mkato*. Kwa kuzingatia majibu hayo, ni dhahiri kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha juu ya tanzu mbalimbali za fasihi. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa ufasaha na hivyo kupata alama za chini.


5 Eleza maana ya dhana zifuatazo

- Shairi - Ni Fasihi Simulizi ambayo huwasilishwa kwa njia ya kuimba au kughani

- Ngonjera - Ni shairi ambalo huwasilishwa kwa njia ya kuimba kwa lengo la kusifia kitu

- Utenzi - Ni bahari ya ushairi ambayo una kipande kimoja cha mshororo

- Kina - Ni Sehemu ya ~~mwisho~~ kati katika ushairi au ni vina vya kati katika shairi

**Kielelezo Na. 5.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 5.2 sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyechanganya dhana za shairi, ngonjera, utenzi na kina kinyume na matakwa ya swali.

### 2.1.6 Swali la 6: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha shughuli nne za wanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maudhui ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Swali lilijibiwa na watahiniwa wote 3,262 waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 94.4 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Uchambuzi wa data unaonesha kuwa, watahiniwa 2,734 sawa na asilimia 83.8 walipata kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hawa waliweza kubainisha shughuli za wanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maudhui ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa hao waliweza kubainisha shughuli hizo kuwa ni *kusikiliza*, *kujibu maswali*, *kuuliza maswali* na *kuchunguza zana*. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.


6 (i) kuchukua nukuu. mwanafunzi huweza kuchukua nukuu kwa Mwalimu kwa kifupi zaidi;

(ii) Kusikiliza kwa makini. pia mwanafunzi anatakiwa awe makini anapofundishwa ili kuelewa maudhui hayo

(iii) Kuhoji au kuuliza sehemu ambayo ajaelewa ili mwalimu amfafanulie vizuri zaidi.

iv) Kueleza mawazo yake juu ya maudhui yanayofundishwa. nivema mwalimu kummhusu mwanafunzi kuchangia jinsi anavyoelewa.

**Kielelezo Na. 6.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6

Kielelezo Na. 6.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubaini na kufafanua kwa kifupi shughuli za wanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maudhui ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kadhalika watahiniwa 345 sawa na asilimia 10.6 walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kuwa waliweza kutaja shughuli mbili za wanafunzi wakati wa ujifunzaji kati ya nne na wengine walitaja shughuli bila kuzitolea ufafanuzi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alibainisha kazi za mwanafunzi kuwa ni; *kuwa na karatasi na kalamu, kuepuka mambo yanayopotosha usikivu* na *kukaa eneo ambalo anamwona mwalimu.* Majibu haya yanaashiria kuwa mtahiniwa huyo ameelewa matakwa ya swali lakini hana maarifa ya kutosha juu ya mada ya "Shughuli za mwanafunzi wakati mwalimu anafundisha".

Watahiniwa 183 sawa na asilimia 5.6 walikuwa na ufaulu hafifu kwa kuwa walipata alama kuanzia 0 hadi 0.5 baada ya kushindwa kubainisha shughuli za wanafunzi wakati mwalimu anafundisha. Watahiniwa walitoa hoja ambazo hazikuwa shughuli za wanafunzi wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kama vile; *kukaa dawati la mbele, kukaa kimya, kufuta ubao* na *kutazama mbele.* Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu katika swali hili.



| | | |
|---|---|---|
| 6. | i) | Ubunifu |
| | (ii) | Uvumbuzi |
| | (iii) | Uwezo wa kufikiri kiyakinifu. |
| | (iv) | Kudadisi |

**Kielelezo Na. 6.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 6

Kielelezo Na. 6.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubaini na kufafanua kazi za mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.1.7 Swali la 7: Utungaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja mambo manne ya kuzingatiwa wakati wa uandishi wa insha na lilitoka katika mada ya Utungaji. Jumla ya watahiniwa 2,498 walijibu swali hili. Asilimia 44.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4 na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yenye ufaulu wa wastani.

Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika swalu la 7.




**Chati Na. 7**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 1,365 sawa na asilimia 55.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 1.5 hivyo kuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Watahiniwa hao, walieleza muundo wa insha badala ya kutaja mambo ya kuzingatia wakati wa uandishi wa insha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja mambo yasiyokuwa sahihi katika uandishi wa insha kuwa ni *mwandiko mzuri, usafi na unadhifu wa insha au kazi, kuandika utangulizi wa insha, kuandika kiini cha insha* na *kuandika hitimisho la insha*. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyo sahihi katika swali hili.



| | | |
|---|---|---|
| 7. | i) Kuandika kichwa cha insha | |
| | ii) Kuandika utangulizi wa insha | |
| | iii) Kuandika kiini cha insha | |
| | iv) Kuandika hitimisho la insha | |

**Kielelezo Na. 7.1**: Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 7

Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja muundo wa insha, badala kutaja mambo manne yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa uandishi wa insha.

Aidha, watahiniwa 778 sawa na asilimia 23.9 walikuwa na ufaulu wa juu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hao waliweza

kutaja mambo ya kuzingatia wakati wa uandishi wa insha kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja kwa usahihi mambo ya kuzingatia unapoandika insha kuwa ni *kukusanya mawazo, kuchambua mawazo, kupanga mawazo na matumizi sahihi ya alama na matumizi ya lugha fasaha*. Majibu haya yanathibitisha kuwa, watahiniwa kutoka katika kundi hili walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya Utungaji hususan kipengele cha uandishi wa insha. Kielelezo Na.7.2 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyejibu swali hili.


7. (i) kuchagua mada.
(ii) kupanga mawazo.
(iii) kuzingatia taratibu za uandishi.
(iv) kutumia lugha fasaha.

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 7

Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja mambo manne yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa uandishi wa insha.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 355 sawa na asilimia 20.8 walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwani waliweza kutaja mambo mawili badala ya mambo manne ya kuzingatia wakati wa uandishi wa insha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutaja hatua mbili kwa usahihi na zingine akashindwa kama ifuatavyo: *kichwa cha insha, utangulizi wa insha, ukusanyaji wa mawazo na lugha fasaha*.

### 2.1.8 Swali la 8: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili

Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa kifupi faida nne za kutumia mbinu ya Masimulizi kufundishia fasihi katika shule za msingi. Swali lilipima tathimini na lilitoka katika mada ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia na lilijibiwa na watahiniwa wote (3,262) waliofanya mtihani huu. Watahiniwa 1,391 sawa na asilimia 42.7 walifaulu kwa kiwago cha wastani kwani walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Uchambuzi wa majibu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 1,391 sawa na asilimia 42.7 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 2 hadi 2.5. Miongoni mwa sababu zilizowafanya watahiniwa kuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu katika swali hili ni kushindwa kutoa hoja nne kulingana na matakwa ya swali na kurudia hoja kwa maelezo tofauti kwa sababu ya kukosa maarifa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika faida nne za kutumia mbinu ya masimulizi kuwa ni: *mbinu ya masimulizi haimchoshi mwanafunzi, mbinu ya masimulizi huchangamsha, mbinu ya masimulizi huvuta ari ya mwanafunzi katika kujifunza* na *haihitaji gharama*. Baadhi ya hoja za mtahiniwa zimejirudiarudia kwa maelezo tofauti lakini pia baadhi sio sahihi hivyo kupata alama za wastani.

Takwimu za majibu ya watahiniwa zinaonesha kuwa, watahiniwa 1,365 sawa na asilimia 41.8 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hawa, walieleza faida za kutumia mbinu zingine za kufundishia badala ya mbinu ya Masimulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa faida za matumizi ya mbinu ya Masimulizi kuwa ni: *huokoa muda, haihitaji pesa za kigeni, mwalimu hutumia muda mfupi kufundisha.* Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


8. Masimulizi:- Ni mbinu inayotumiwa na mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji ambapo wanafunzi huwa ni wasikilizaji au wapokeaji wa kile kinachosimuliwa
i/ Huokoa muda katika ufundishaji
Mbinu hii inapokuwa inatumiwa, inaokoa muda kwani haimpi uhuru mwanafunzi kuteta
ii/ Mambo mengi huweza kufundishwa au kusimuliwa
Pia [illegible] wa kufundisha mambo mengi ni mkubwa kwani mtendaji mkuu ni mwalimu katika usimuliaji.
iii/ Hupunguza maswali mengi
Pia kutokana na mbinu hii haimshirikishi mwanafunzi, huweza kusaidia kupunguza idadi ya maswali.
iv/ Haina gharama
Mbinu hii inapotumiwa hupunguza gharama kwani humuitaji mwalimu na hadithi yake ili kuweza kusimulia kwa wanafunzi.

**Kielelezo Na. 8.1**: Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 8

Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza faida za kutumia mbinu nyingine za ufundishaji badala ya mbinu ya Masimulizi kufundishia mada ya fasihi kwa shule za msingi.

Hata hivyo, watahiniwa 506 ambao ni sawa na asilimia 15.5 walijibu swali hili kwa usahihi na kufaulu kwakupata alama kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hao, waliweza kufafanua faida nne za kutumia mbinu ya masimulizi kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya mbinu za Kufundisha na Kujifunzia Kiswahili. Hivyo, kuweza kufafanua faida za mbinu ya Masimulizi. Wengine waliweza kueleza faida tatu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja faida hizo kuwa ni: *husaidia kujenga ushirikiano kati ya mwalimu na wanafunzi, humjengea mwanafunzi uwezo wa kujieleza, humjengea mwanafunzi hali ya kujiamaini, hujenga mahusiano mazuri na upendo kati ya anayesimulia na wanaosikiliza*. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.



8. i) Husaidia kuvuta usikivu wa darasa. Hali hiyo hupelekea kulitawala na kulimudu darasa na kufanya somo liweze kuokowa kwa haraka.

ii) Kuwajengea wanafunzi kumbukumbu za muda mrefu. Kupitia mbinu ya masimulizi wanafunzi wataweza kutunza kumbukumbu na kuwa na uwezo wa kurejelea yale waliyosoma/waliyofundishwa.

iii) Wanafunzi kulipenda na kulifurahia somo kutokana na mbinu ya masimulizi wanafunzi watalipenda somo kwa sababu wanafunzi wengi hupenda kusimuliwa mambo mbalimbali.

iv) Kukuza stadi mbalimbali za lugha. Mfano ~~kusik~~ stadi ya kusikiliza na kuzungumza huweza kukuzwa na kujengwa kwa wanafunzi.

**Kielelezo Na. 8.2**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8

Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua faida ya matumizi ya mbinu ya Masimulizi katika kufundishia mada ya fasihi kwa shule za msingi.

### 2.1.9 Swali la 9: Ufahamu

Swali lilimtaka mtahiniwa aorodheshe mambo manne ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari iliyosikilizwa au kusomwa. Swali lilikuwa maalum kupima ufahamu wa mtahiniwa. Swali lilijibiwa na watahiniwa 2,880. Watahiniwa 2,226 sawa na asilimia 68.2 waliofanya swali hili walipata ufaulu wa wastani na kuendelea kuanzia alama 2 hadi 2,5. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 1,450 sawa na asilimia 44.4 walifaulu kwa kupata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kutokana na sababu zifuatazo: Watahiniwa waliweza kutaja kwa usahihi baadhi ya hoja na walishindwa hoja nyingine na watahiniwa wengine walitaja kanuni au mbinu ya kuzingatia wakati wa kufundisha kusoma kimya/sauti kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi kuwa ni: *kuwepo na mzungumzaji na msikilizaji, kuzingatia matumizi ya lugha fasaha, kuzingatia alama za uandishi* na *kuwa na mtiririko mzuri wa mawazo*. Hoja hizo kwa upande mmoja zinaeleza kanuni za uandishi wa insha lakini upande mwingine zinataja sifa za kusoma kimya au kwa sauti hivyo alipata alama za wastani.

Pamoja na hayo, watahiniwa 654 sawa na asilimia 31.8 walifaulu kwa kupata alama 0 hadi 1.5. Hivyo, swali lilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa katika kundi hili walishindwa kubaini tofauti ya mambo ya kuzingatiwa ili kupata ujumbe wakati wa kusoma au kusikiliza na mambo ya kuzingatia wakati wa kusoma kimya au kwa sauti. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja mambo hayo kimakosa kuwa ni: *umuhimu wa jambo hilo, kusoma kwa kurudiarudia, kutokuwa na msongo wa mawazo* na *kuzingatia kanuni za kisarufi*. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu katika swali hili.


9. Mambo ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari iliyosomwa au inayosikilizwa.
(a) eneo la kupokelea taarifa lina utulivu wa kutosha
(b) kuepuka vurugu za kimaono kama vile hasira na woga
(c) kuwa tayari kupokea ujumbe uliokusudiwa katika habari
(d) kutilia maanani kile kinachosomwa au kusikilizwa kutoka kwenye habari hiyo

**Kielelezo Na. 9.1**: Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 9

Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja kanuni za kusoma kimya au kwa sauti badala ya kutaja mambo ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa.

Watahiniwa 776 (23.8%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu ambapo walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao waliweza kutaja mambo ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja mambo hayo kuwa ni: *kusikiliza kinachosimuliwa au kinachosomwa, kuhusianisha kinachosomwa na habari inayosimuliwa, mazingira na kubainisha mawazo makuu.* Majibu haya yanaashiria kuwa, watahiniwa waliweza kuelewa matakwa ya swali pamoja na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Ufahamu ambapo waliweza kutaja mambo manne ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu.


9. (i) Kumakinikia habari
(ii) Kufuata matamshi ya mzungumzaji
(iii) Kuhusisha mambo muhimu na habari na inayosomwa.
(iv) Kubaini mawazo makuu.

**Kielelezo Na. 9.2**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 9

Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja mambo ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa.

### 2.1.10 Swali la 10: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa muhtasari hasara nne za kutokutumia zana za kufundishia na kujifunzia wakati wa ufundishaji. Watahiniwa 3,262 walijibu swali hili. Swali lilikuwa mahsusi kupima maarifa na lilikuwa ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Watahiniwa 3,229 sawa na asilimia 99 walipata ufaulu wa wastani na mzuri. Chati Na. 10 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali la 10.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 2,219 ambao ni sawa na asilimia 68 walikuwa na kiwango cha juu cha ufaulu kwa kupata alama 2 hadi 4. Watahiniwa hao waliweza kuelezea kwa usahihi hasara za kutotumia zana za kufundishia na kujifunzia wakati wa ufundishaji. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na watahiniwa ni pamoja na: *kupungua kwa mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi darasani, kupungua kwa usikivu* na *mwalimu kushindwa kuelezea jambo*. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili.


10. (i) Wanafunzi kutokuelewa somo kwa haraka.
⇒ Zana za kufundishia na kujifunzia hurahisisha ufundishaji. kwahiyo zisipotumika ufundishaji na ujifunzaji huwa mgumu.

(ii) Wanafunzi kutokutunza kumbukumbu ya muda mrefu.
⇒ Zana za kufundishia na kujifunzia husaidia wanafunzi kutunza kumbukumbu ya muda mrefu. Hivyo isipotumika husababisha watoto kutokuwa na kumbukumbu.

(iii) Wanafunzi kutokupenda somo.
⇒ Mwalimu asipotumia zana watoto watashindwa kuelewa vizuri somo lake mwishoe wanafeli. Hivyo watalichukia somo.

(iv) kutumia muda mwingi kueleleza jambo dogo. Mwalimu asipotumia zana lazima awe na maelezo mengi ili wanafunzi waelewe. Hivyo anatumia muda mwingi kueleza jambo moja tu.

**Kielelezo Na. 10.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 10

Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza hasara za kutokutumia zana za kufundishia na kujifunzia wakati wa ufundishaji.

Uchambuzi wa kina wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 1,010 sawa na asilimia 31 walipata kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Watahiniwa hawa waliweza kueleza kwa usahihi baadhi ya hasara za kutokutumia zana za kujifunzia na kufundishia na kushindwa kueleza hasara nyingine. Pia, wapo waliotoa majibu yanayofanana kwa kurudia hoja kwa maelezo tofauti. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kujibu kwa usahihi hoja mbili kama ifuatavyo: *kutoweza kuibua hisia za wanafunzi*, *kusababisha kutofikiwa kwa malengo* hivyo alipata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa 33 ambao ni asilimia 1 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 1 hadi 1.5. Baadhi yao walichanganya neno kutumia na neno kutotumia hivyo, walieleza hasara za *kutumia* zana za kufundishia badala ya hasara ya *kutokutumia* zana za kufundishia kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hasara hizo kama ifuatavyo: *kuweza kuibua hisia za wanafunzi, kufikiwa kwa malengo ya somo, kusababisha uchafu ndani ya darasa na kusababisha usumbufu au kelele*. Majibu ya mtahiniwa yanadhihirisha kuwa hakuelewa matakwa ya swali na hawakuwa na maarifa kwani baadhi ya majibu aliyoyatoa hayana uhusiano na matumizi ya dhana kama ilivyokusudiwa. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu katika swali hili.



10. Zana za kufundishia na kujifunzia;
Ni kitu/vitu anavyotayarisha mwalimu
ili vimsaidie katika kuimarisha ma-
rifa kwa wanafunzi wakati wa mcha-
kato wa ufundishaji na ujifunzaji.
Athari za zana za kufundishia
na kujifunzia ni pamoja na:
(1) Hupoteza muda.
— Matumizi ya zana huweza kupotez
a muda mwingi wakati wa ufundishaji.
ii Huweza kusababisha ajali.
— Kuna baadhi ya zana zi huwa ni
hatarishi kwa wanafunzi mfano -
matumizi ya vifaa vya kielektroniki
kama vile TV, huweza kusababisha
shoti
iii Huweza kuchanganya wanafunzi.
— Mwalimu anaweza kuandaa zana
ambazo ina vitu vingi hivyo kuwacha-
nganya wanafunzi.
iv Huweza kusababisha kutokufikiwa
kwa malengo mahususi ya somo

**Kielelezo Na. 10.2**: Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 10

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu yaliyohitaji majibu marefu (Insha) ambayo yalitungwa kutoka katika mada za Taaluma ya Kiswahili. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali mawili (2) ambapo kila swali lilikuwa na uzito wa alama 15. Hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 30. Katika sehemu hii ufaulu wa watahiniwa umegawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alipata kiwango hafifu cha ufaulu endapo alipata alama 0 hadi 5.5, wastani endapo alipata alama 6 hadi 10 na kiwango kizuri cha kufaulu iwapo alipata alama 10.5 hadi 15.

### 2.2.1 Swali la 11: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili na lilimtaka mtahiniwa kueleza sifa nne za fasihi Simulizi. Swali lililenga kupima uchambuzi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3,180. Watahiniwa 3,033 sawa na asilimia 95.4 ya waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani na mzuri kwa kuwa walipata alama kuanzia 6 hadi 14.5. Swali hili lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 11 inafafanua viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 1,537 sawa na asilimia 48.3 walipata alama nzuri kuanzia 10.5 hadi 14.5 hivyo kuwa na kiwango cha juu cha ufaulu. Watahiniwa katika kundi hili waliweza kueleza kwa mifano sifa za fasihi simulizi kutokana na weledi mkubwa waliokuwa nao kuhusu fasihi simulizi. Hata hivyo, watahiniwa wengine walitoa hoja sahihi na kuzielezea lakini hawakuandika utangulizi wala hitimisho, baadhi yao walitoa hoja kwa usahihi lakini walishindwa kuzielezea kwa kina baadhi ya sifa za fasihi simulizi na wachache walifanikiwa kuelezea sifa nyingi kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa sifa za fasihi simulizi kama vile; *uwepo wa uwanja wa kutendea, uwepo kwa hadhira, uwepo wa fanani* na *huwa ni mali ya jamii nzima* kisha alitoa utangulizi na hitimisho hivyo, alipata ufaulu mzuri. Kielelezo Na.11.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa ufasaha swali hili.



11 Fasihi simulizi; Ni aina ya fasihi ambayo huwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Mfano wa fasihi simulizi ni hadithi na masimulizi mbalimbali. Zipo sifa mbalimbali ambazo zinaweza kuifanya fasihi simulizi kuwa ni tofauti na fasihi andishi. Zifuatazo ni sifa za fasihi simulizi;

Huwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo; Katika fasihi simulizi fanani na hadhira yake hukutana na kuzungumza ana kwa ana. tofauti na fasihi andishi ambapo fanani na hadhira hawawezi kuonana ana kwa ana. Mfano; Mtu anaposimulia hadithi na watu wanamsikiliza kwa makini ni sifa moja wapo ya fasihi simulizi.

Fasihi simulizi huweza kupokea mabadiliko ya papo hapo; Hii pia ni sifa ya fasihi simulizi. Fasihi simulizi huweza kupokea mabadiliko ya papo hapo wakati wa masimulizi. tofauti na fasihi andishi ambayo haiwezi kupokea mabadiliko ya haraka mpaka litolewe toleo lingine. Mfano fanani anaposimulia hadithi fulani huweza kukosolewa na kubadilisha maneno kwa muda huohuo.

Fasihi simulizi huzaliwa, hukua na hufa; Hii inatokana na pale watu wanapoipokea na kuiendeleza katika jamii tofauti. Hivyo inakuwa imekua. Vilevile ~~kwa~~ fasihi simulizi huweza kufa pale watu wanapokuwa hawana muda wa kuiendeleza ili iendelee kukua hivyo hupotea kabisa katika jamii. Mfano fasihi simulizi inapowasilishwa na hadhira

**Kielelezo Na. 11.1**: Sampuli ya Sehemu ya Majibu Sahihi katika Swali la 11

Kielelezo Na. 11.1: Ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi kwa kueleza sifa za fasihi simulizi.

Hata hivyo, Watahiniwa 1,496 sawa na asilimia 47.1 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao waliweza kueleza baadhi ya sifa za fasihi simulizi na kushindwa sifa nyingine, wengine walifanikiwa kueleza sifa chache za fasihi simulizi na hawakuandika hitimisho la kazi zao. Kadhalika, watahiniwa wachache walitaja sifa za fasihi simulizi bila kuzitolea maelezo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa sifa sahihi za fasihi simulizi kama vile; *sifa ya utendaji* na *uwepo wa fanani* lakini akatoa sifa zisizosahihi kama vile, *ni mali mtu mmoja* na *haina gharama* yoyote hivyo, alipata ufaulu wa wastani.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 147 sawa na asilimia 4.6 walipata alama hafifu kwa kuwa walitoa wahusika wa fasihi simulizi badala ya sifa za fasihi simulizi. Watahiniwa wengine walieleza njia za uhifadhi wa fasihi simulizi na wachache walieleza dhima za fasihi simulizi badala ya kueleza sifa za fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa sifa zisizosahihi za fasihi simulizi kama vile; *wanyama, vitu na mahali, binadamu, fanani* na *hadhira*. Kielelezo Na.11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.



11. fasihi simulizi; Ni kuna ya fasihi ambayo huwasilishwa kwa njia ya mdomo mfano hadithi au masimulizi. Fasihi simu lizi ina sifa zifuatazo.

Ni mali ya jamii nzima; Fasihi sim ulizi hutolewa kwa njia ya mdomo kimasi mulizi kwa rika zote wakubwa na wadogo ambao wanaojua kusoma na wasiojua kuso ma ili mradi wote waweze kupata masimu lizi hayo yakuwa yanatolewa. Huyo basi ni mali ya jamii nzima.

Ubunidisha jamii; kutokana na kuwepo na watu wenye vipaji mbalimbali vya masimulizi mfano Babu au bibi wana pokuwa wanasimulia hadithi za zamani za kale hii inapelekea kubunidisha hadhira yake wanapokuwa wakimsikiliza Huyo ni moja ya faida za fasihi simulizi.

Uelimisha jamii juu ya mambo mbalimbali; Fasihi simulizi inaelimisha juu ya vitu vingi mfano uvutaji wa madaw a ya kulevya ni hatari kwa afya yako hivyo si vizuri kwa utapata madonjwa ya moyo. Huyo basi fanani anapokuwa anatoa simulizi yake inapelekea kuelimish a jamii yake kwa kupitia hadhira wanaomsikiliza

Hukosoa na kuonya jamii; kutokana na masimulizi mbalimbali ya watunzi au wasanii wetu wanapokuwa wanasim ulia hadithi zao juu ya mambo mbali mbali mfano ukeketaji wa watoto wa

**Kielelezo Na. 11.2**: Sampuli ya Sehemu ya Majibu Yasiyosahihi katika swali la 11

Kielelezo Na. 11.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza dhima za fasihi simulizi badala ya sifa za fasihi simulizi.

### 2.2.2 Swali la 12: Stadi za Lugha

Swali lilitoka katika mada ya Stadi za Lugha na lililenga kupima tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa kutetea hoja kuwa Lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano katika jamii. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 2,859 walijibu swali hili. Miongoni mwao, watahiniwa 2,704 sawa na asilimia 94.6 ya waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa walipata alama kuanzia 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12*

Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 1,971 sawa na asilimia 69 walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao waliweza kueleza baadhi ya umuhimu wa lugha kwa jamii na kushindwa kueleza umuhimu mwingine wa lugha. Watahiniwa wengine walifanikiwa kuelezea umuhimu wa lugha kwa jamii lakini hawakuandika utangulizi wa kazi zao. Vile vile, watahiniwa wachache walitaja umuhimu wa lugha kwa jamii bila kutolea maelezo hoja zao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa umuhimu wa lugha kwa jamii kama vile; *hurithisha mila na desturi za jamii, huelimisha* na *hujenga mahusiano ya wanajamii* lakini akatoa umuhimu wa lugha usiosahihi kama vile, *lugha hutumika katika kampeni za kisiasa* na *lugha hutumika katika biashara* hivyo, alipata ufaulu wa wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 733 sawa na asilimia 25.6 walipata alama nzuri kuanzia 10.5 hadi 15 hivyo walikuwa na kiwango cha juu cha ufaulu. Watahiniwa hawa waliweza kueleza kwa mifano umuhimu wa lugha kwa jamii kutokana na ujuzi mkubwa waliokuwa nao kuhusu lugha. Watahiniwa wengine walitoa hoja sahihi na kuzielezea lakini hawakuandika hitimisho, baadhi yao walitoa hoja kwa usahihi lakini walishindwa kuelezea baadhi ya hoja hizo na wachache walifanikiwa kutoa hoja kuhusu umuhimu wa lugha kwa jamii kwa usahihi na kuzielezea kikamilifu hivyo walipata alama zote 15. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa umuhimu wa lugha kwa jamii kama vile; *hurithisha amali za jamii, hutambulisha utamaduni wa watu, hujenga mahusiano ya watu, huelimisha* na *huunganisha wanajamii*. Kielelezo Na.12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili.



12. Lugha: Ni mfumo wa sauti za nasibu zenye kubeba maana iliyokubaliwa na kutumika katika mawasiliano. Zifuatazo ni faida za Lugha kuwa chombo muhimu cha mawasiliano katika jamii

Hutumika kutambulisha jamii: Lugha ni chombo cha mawasiliano kwa sababu hutumika kutambulisha jamii fulani hii imetokana na kwamba kila jamii ina Lugha yake inayoitambulisha jamii hiyo mfano jamii ya Wamasai inatumia kimasai katika mawasiliano yao ya kila siku japo Lugha halali iliyothibitishwa na kuidhinishwa itumike katika mawasiliano ni Kiswahili Lakini Lugha za asili ndiyo inayoitambulisha jamii husika.

Hutumika katika kujifunzia na kufundishia: Pia Lugha kama chombo cha mawasiliano Inatumiwa na walimu katika kuwafundisha wanafunzi na pia wanafunzi wanaitumia Lugha katika kujifunzia mambo mbalimbali na wao wenyewe kuitumia katika mawasiliano ili waweze kuelewana.

Hutumika katika kudumisha uhusiano mwema; Lugha inamanufaa makubwa kwani inatumika katika kujenga uhusiano mwema miongoni mwa jamii mfano mfanya biashara anapofanya shughuli zake za kila siku anatumia Lugha kuwasiliana na wateja wake ili kuweza kudumisha uhusiano mwema miongoni mwao.

Hutumika kujenga umoja na mshikamano: Pia Lugha kama chombo cha mawasiliano inatumika katika kujenga umoja na mshikamano hii inatokana na watu kuwasiliana vizuri na kushirikiana vema katika kutekeleza majukumu au shughuli mbali

**Kielelezo Na. 12.1**: Sehemu ya Majibu Sahihi katika Swali la 12

Kielelezo Na. 12.1: kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza umuhimu wa lugha kwa jamii.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 155 sawa na asilimia 5.4 walipata alama hafifu. Watahiniwa hawa hawakuandika utangulizi na hitimisho na walitoa matumizi ya lugha badala ya umuhimu wa lugha. Watahiniwa wengine walitoa hoja mbili sahihi lakini walishindwa kuzitetea ipasavyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa umuhimu wa lugha kama vile; *hutumika katika biashara, hutumika katika elimu, hutumika katika bunge, hutumika katika siasa* na *hutumika vitani* kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na.12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kama inavyotakiwa.



12. Lugha; Ni sauti za nasibu ambazo hutumika na kundi fulani la watu na kuweza kuelewana kwa matamshi na lafudhi zao. Ufuatao ni umuhimu wa lugha kama chombo cha mawasiliano katika jamii.

Hurahisisha mawasiliano baina ya watu wa jamii fulani; Lugha ndio chanzo kikuu katika mawasiliano hivyo husaidia katika kurahisisha mawasiliano baina ya makabila tofauti tofauti hivyo ni chombo cha mawasiliano.

Kukua na kuongezeka kwa msamiati katika Kiswahili; Kutokana na kuwa ndio chanzo kikuu cha mawasiliano katika jamii kumepelekea kukua na kuongezeka msamiati mbalimbali ya lugha katika kiswahili.

Kukuza stadi ya mazungumzo; Lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano katika jamii ambacho kimekuza stadi ya mazungumzo kupitia lugha mbalimbali zilizopo Afrika na Tanzania.

Kukua na kuenea kwa sayansi na teknolojia; Kutokana na kuwepo na mawasiliano baina ya nchi mbalimbali hii imepelekea kuenea kwa sayansi na teknolojia nchini kwa kupitia chombo cha mawasiliano ambacho ni sauti za nasibu kama lugha. Hivyo basi lugha ina umuhimu katika jamii kama chombo cha mawasiliano.

**Kielelezo Na. 12.2**: Sampuli ya Sehemu ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 12

Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

### 2.2.3 Swali la 13: Utungaji

Swali lilitoka katika mada ya Utungaji kipengele cha Alama za Uandishi ambapo mtahiniwa alitakiwa atumie mifano kueleza matumizi matatu kwa kila alama ya uandishi aliyopewa kama vile: (a) Nukta (b) Mkato (c) Alama ya kuuliza (d) Nukta na mkato (e) Mshangao. Swali lilikuwa mahsusi kupima maarifa.

Swali lilijibiwa na watahiniwa 489. Miongoni mwao, watahiniwa 423 sawa na asilimia 86.5 walijibu vizuri swali hili kwa kuwa walipata alama nzuri kuanzia 6 hadi 14. Chati Na.13 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali la 13.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 109 sawa na asilimia 22.3 walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 14 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya Utungaji hususan Alama za Uandishi. Watahiniwa waliweza kueleza matumizi matatu kwa kila alama za uandishi walizopewa. Aidha, baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa yalikuwa kama vile; Nukta (.) *hutumika katika kuandika tarehe mfano 04.05.2021, hutumika kuonesha mwisho wa sentensi mfano, baba analima; hutumika kuonesha pumziko kubwa mfano Fisi na Sungura walikuwa marafiki wa siku nyingi sana.* Mkato (,) *hutumika katika kuonesha pumziko dogo mfano baba na mama walikwenda shambani asubuhi na mapema, wakakutana na mwizi alfajiri hiyo; hutumika kutenganisha vitu mbalimbali mfano kikombe,*

*kiti, meza* na *bakuli;* Alama ya Kuuliza (?) *hutumika katika kuuliza maswali mbalimbali* mfano, *Umekula chakula kiasi gani?, hutumika kuonesha mwisho wa sentensi au habari mfano Umejifunza nini kutokana na kisa hiki?, hutumika kuonesha hali ya Mshangao mfano Unasemaje?!;* Nukta na mkato (;) *hutumika kuandika vitu vinavyohitajika* mfano, *Niletee vitu vifuatavyo; nyanya, mafuta na vitunguu, hutumika kuunganisha sentensi mbili au zaidi mfano Baba alikuwa analima shambani; mama alikuwa anapika chakula shambani.* Mshangao (!) *hutumika kuonesha hisia* kama *kushangaa juu ya jambo fulani mfano Haah! anaondoka?.* Kielelezo Na.13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.

13. (a) Nukta (.)

(i) Hutumika kuandikwa mwisho wa sentensi au habari.

Mfano. Baba anapika na Mama analima.

(ii) Hutumika kutenganisha maneno yaliyofupishwa.

Mfano. Sanduku la Posta (S.L.P)

(iii) Hutumika kuonesha mapumziko katika usomaji wa habari au hadithi.

(b) Alama ya kuuliza (?)

(i) Hutumika katika uulizaji wa maswali.

Mfano. Kweni ni wapi?

(ii) Hutumika katika kuhakiki kauli mbalimbali.

Mfano. Je ameleta?

(iii) Hutumika katika kuonesha mshtuko/kustajabu.

Mfano. Kweli ameaga dunia?

(c) Mshangao (!)

(i) Hutumika kuonesha masikitiko juu ya jambo fulani.

Mfano. Looo!!!

(ii) Hutumika katika kuonesha hali ya kusisitiza.

Mfano. Urudi hapa haraka!

(iii) Hutumika kuonesha mshangao juu ya jambo fulani.

Mfano. Mbuzi analiwa!!


13. (b) Mkato (,)
(i) Hutumika kutenganisha kitu kimoja na kingine.
Mfano. Simba, chui, mamba, nyani na twiga ni wanyama wa porini.
(ii) Hutumika kuonesha mapumziko mafupi wakati wa usomaji wa hadithi au habari.
(iii) Hutumiwa na watungaji wa mashairi kutenganisha vina vya kati na vya mwisho.
Mfano. Tujikinge na ukimwi, Gonjwa hili ni hatari,
(d) Nukta na mkato (;)
(i) Hutumika kuonesha mapumziko mafupi wakati wa usomaji wa hadithi au habari.
(ii) Hutumika kutofautisha sentensi moja na nyingine.
(iii) Hutumika katika uandishi wa magazeti.
Mfano. (ajira zatangazwa;)

**Kielelezo Na. 13.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 13

Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza matumizi ya alama za uandishi kwa ufasaha.

Halikadhalika, watahiniwa 314 sawa na asilimia 64.2 walifaulu swali kwani walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10 kutokana na sababu zifuatazo: baadhi waliweza kueleza matumizi ya alama za uandishi bila kuonesha mifano. Aidha, wengine walielezea kwa kina baadhi tu ya vipengele na walishindwa katika vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu sahihi kama vile; Nukta na mkato (;) *hutumika kuandika vitu vinavyohitajika mfano Niletee vitu vifuatavyo; nyanya, mafuta na vitunguu, hutumika kuunganisha sentensi mbili au zaidi mfano, Baba alikuwa analima shambani;mama alikuwa anapika chakula shambani.* Mshangao (!): *hutumika kuonesha hisia kama kushangaa juu ya jambo fulani mfano, Haah! anaondoka?* lakini alitoa majibu yasiyo sahihi kama vile; *kuonesha mdokezo, kuonesha uachano fulani* na *kuonesha muachano wa nafasi.* Hivyo, alipata ufaulu wa wastani.

Hata hivyo, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 66 sawa na asilimia 13.5 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa hao walipata ufaulu wa chini kwa sababu hawakufuata maelekezo ya swali ambalo lilimtaka mtahiniwa atumie mifano kueleza matumizi matatu ya kila alama ya uandishi aliyopewa. Watahiniwa hawa walieleza matumizi machache yaani moja hadi mawili ya alama za uandishi kinyume na mahitaji ya swali. Aidha, watahiniwa wengine hawakuwa na uelewa mzuri juu ya matumizi ya alama za uandishi hali hii ilisababisha kushindwa kutoa ufafanuzi sahihi kuhusu alama za uandishi. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi ya watahiniwa yalikuwa*;* Nukta (.) *hutumika mwishoni mwa sentensi au mwanzoni mwa sentensi kwa kutenganisha kituo cha kwanza na kituo kingine mfano, mtoto mzuri alikuwa anacheza.* Mkato (,) *hutumika popote kwenye sentensi*, Alama ya kuuliza (?) *hutumika katika uandishi endapo mwandishi atakuwa anahitaji kuuliza swali kwenye habari yake mfano, alikwenda wapi?* Nukta na Mkato (;) *hutumika katika uandishi wakati wa kutenga aya moja na aya nyingine*. Mshangao (!) *hutumika pale mwandishi anapokuwa anatumia maneno ya mshangao* na mara nyingi alama hii *hutumika popote kwenye uandishi iwe ni mwanzo, katikati au mwisho.* Hivyo, alipata ufaulu wa chini. Kielelezo Na. 13.2 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa.



13 (a) Nukta
Matumizi ya nukta
(i) Kuonesha mwisho wa sentensi pale ambapo sentensi inaishia mwishoni tunaweka nukta mfano
mfano Wanafunzi wote wameagizwa Majembe.
(ii) Inaonesha Muachano kati ya sentensi moja na nyingine kwa mfano
Nitakuja kesho kutwa ila kukosa. Sitakosa kabisa kuhudhuria kikao.
(iii) Inatumika kuonesha pumziko refu mfano refu
mfano wa pumziko refu
Hivyo basi tutakutana kesho kutwa.
(b) Mkato (,)
Matumizi
(i) Inaonesha pumziko dogo
mfano
Nimetembelea hospitalini, Nikarudi haraka
(ii) Inaonesha Utengano / uachano wa Maneno fulani
mfano Machungwa, Maembe, mananasi,
13 b - Pia hutumika katika kwa waongeaji ambapo msongi huweza kupumzika kwa lkini huwa si sana kama ilivyo kwenye nukta.
13 c) Alama ya kuuliza ?
- Hutumika kutumika sana sana katika uulizaji wa maswali mbalimbali mfano.
Yuwapi Juma ?
13 d) Nukta na mkato ;
- Hutumika katika maelezo mbalimbali mfano:
Elimu ; Nilisoma kuanzia miaka (5) na kuendelea.
13 e) Mshangao !
- Hutumika kuonesha hisia za mshituko ya ndani ya waongeaji mfano:
- Loh!
- Kumbe!
- Alaa!
- Pia mshangao huweza kutumika katika maandiko mbalimbali ambapo mwandishi huweza kutumia ili kuonesha hisia zake mfano:
Alee kumbe!
Alaa kumbe ni mwanao!!

Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 13

Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi vipengele vichache na kushindwa katika vipengele vingi kuhusu alama za uandishi.

## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) yaliyohitaji majibu marefu (Insha) ambayo yalitungwa kutoka katika mada ya Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali mawili (2). Kila swali lilikuwa na uzito wa alama kumi na tano (15) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 30. Katika sehemu hii ufaulu umegawanyika katika makundi matatu yaani alama 0 hadi 5.5 vizuri, alama 6 hadi 10 wastani na alama 10.5 hadi 15 hafifu.

### 2.3.1 Swali la 14: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili lilitoka katika mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia. Swali lililenga kupima maarifa. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua namna nne na faida mbili za kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3,156 ambao ni sawa na asilimia 96.8 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu. Watahiniwa 3,130 sawa na asilimia 99.2 walifaulu kwa kiwango kizuri kwani, walipata alama kuanzia 6 hadi 14.5. Chati Na.14 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali la 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 2,878 sawa na asilimia 91.2 walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 14.5. Hii ilitokana na sababu zifuatazo: baadhi ya watahiniwa walitoa hoja zote na kuzifafanua kikamilifu lakini hawakuandika utangulizi wala hitimisho katika kazi yao. Pia, watahiniwa wengine waliweza kufafanua namna nne na faida mbili za kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia na kutoa mifano maridhawa. Kielelezo Na.14.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata ufaulu wa juu.

14. Zana za kufundishia na kujifunzia ni nyenzo zinazo tumiwa na mwalimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Kuna aina kuu mbili za zana ambazo ni asilia na za kisasa. Pia yako makundi matatu ya zana ambayo ni zana masikizi, zana maono na zana masikizi maono.

Zifuatazo ni namna za kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia.

Kuweka kwenye chumba maalumu ambacho hakina unyevu, njia au namna mojawapo ambayo inaweza kutumiwa ili kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia ni kuzitunza kwenye chumba maalumu ambacho chumba hicho hakiwezi kuwa na unyevu ambao unasababisha kuharibika kwa zana hizo ya kufundishia na kujifunzia. Kwa kufanya hivo zana zitadumu lakini ukitunza sehemu zenye unyevu lazima iharibike.

Kutunza kwenye kabati, ni muhimu kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia baada ya kumaliza kutumia vifaa hivyo. Kwa kutunza vifaa vyako au zana kwenye kabati itakusaidia mwalimu pia kuipata kwa haraka pia kuokoa gharama hivyo ni muhimu kuwepo na makabati mbali mbali ambayo yatasaidia kuhifadhi zana baada ya kumaliza matumizi yake.

Kubandika ukutani, pia njia nyingine inayoweza kutumika katika kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia baada ya kumaliza kuzitumia ni kuzibandika ukutani kama kumbukumbu ambayo itawasaidia wanafunzi waendelee kuitumia hivyo kufanya zana iendelee kua katika hali ya usalama.



14. Kutunza kwenye ~~kabat~~ boksi, ni muhimu kuhifadhi zana au vifaa baada ya kumaliza kuvitumia vifaa hivyo. Kuhifadhi kwenye boksi ni moja ya njia itakayosaidia kutunza zana au vifaa baada ya kumaliza mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji hivyo ni vyema ukimaliza kutumia vifaa vihifadhi katika boksi.

Zifuatazo ni faida zinazopatikana kutokana na kuhifadhi zana za ufundishaji na ujifunzaji.

Inafanya zana zidumu kwa muda mrefu, ni vyema kuhifadhi zana baada ya kumaliza kuzitumia kwa sababu inafanya zana hizo zidumu kwa muda mrefu hivyo zinaweza kuendelea kutumiwa zaidi na zaidi katika ufundishaji.

Huokoa gharama, ni muhimu kuhifadhi zana au vifaa baada ya kumaliza kutumia kwa sababu huokoa gharama kwa sababu ukitunza vifaa vyako vya kufundishia unaweza pia kutumia katika kufundishia masomo au kwa matumizi mengine.

Hivyo basi hizo ni faida za kuhifadhi zana au vifaa baada ya kumaliza kuzitumia pamoja namna ya kuhifadhi zana hizo ili zisiweze kuharibika kwa haraka.

**Kielelezo Na. 14.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 14

Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua namna nne na faida mbili za kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia.

Hata hivyo, watahiniwa 252 sawa na asilimia 8 ya waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10 kwani watahiniwa wengi waliweza kufafanua baadhi tu ya namna za kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia na wakashindwa kufafanua namna nyingine. Pia, wengine hawakuandika utangulizi, hitimisho wala faida za kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia. Aidha, wapo waliotoa hoja zao bila kuzitolea maelezo kutokana na kukosa weledi wa kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia. Hivyo, kupata alama za wastani.

Kadhalika, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 26 sawa na asilimia 0.8 walipata alama hafifu kwa kuwa walifafanua njia za upatikanaji wa zana badala ya kueleza namna za kuhifadhi zana za

kufundishia na kujifunzia na faida zake. Baadhi ya majibu yaliyotolewa na watahiniwa yalikuwa kama ifuatavyo; *Kufaragua, kuchonga, kutengeneza, kununua, kuazima* na *kuchora.* Majibu mengine yaliyotolewa yalihusu umuhimu wa kutumia zana za kufundishia na kujifunzia mfano, *kuwajengea uwezo wa kudadisi wakati wa kujifunza, kuleta usikivu darasani.* Kwa upande wa faida za kutunza zana watahiniwa walieleza kuwa ni *kujenga mahusiano mema kati ya mwalimu na wanafunzi* na *husaidia kukuza mila na desturi*. Majibu kama haya hayana uhusiano na swali lililoulizwa. Kielelezo Na. 15.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyosahihi.


14 Zana za kufundishia na kujifunzia: Ni
jumla ya vifaa anavyo viandaa mwalimu
ili ~~aweze~~ avitumie na vimsaidie kati-
ka kufanikisha mchakato mzima wa
ufundishaji na ujifunzaji uwapo da-
rasani.
Yafuatayo ni matumizi ya zana
za kufundishia na kujifunzia somo
la kiswahili.
Kuwajengea wanafunzi kumbu-
kumbu za kudumu. Mwalimu anapo
fundisha somo lake kwa kutumia zana
husaidia katika kuwajengea wana-
funzi kumbukumbu za muda mrefu
kwa kile walicho fundishwa siku hiyo
na ~~[illegible]~~ zana iliyo tumika.
Huwajengea wanafunzi ari na
shauku ya kulipenda somo. Wanafu-
nzi hupenda sana kujifunza kwa na
dharia na vitendo hivyo basi mwali-
mu atumiapo zana kufundishia somo
huwavutia sana wanafunzi na kupe-
lekea wanafunzi kulipenda somo
hilo na mwalimu wao kwa ujumla
kwa kuwa mwalimu huwashirikisha
wanafunzi wake kwenye somo.
Huwajengea wanafunzi uwezo
wa kubuni na kudadisi wakati
wa kujifunza. kupitia kuona zana alizo-
ziandaa mwalimu wanafunzi humuiga
mwalimu alivyo tengeneza zana zake
na kutumia zana katika kuhakikisha
kwa malengo makuu ya somo ya-
nafikiwa na wanafunzi wanashiri-
ki kikamilifu katika mchakato mzi-
ma wa ufundishaji na ujifunzaji
wa somo.

**Kielelezo Na. 14.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 14

Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua matumizi ya zana za kufundishia na kujifunzia badala ya kufafanua namna nne na faida mbili za kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia.

### 2.3.2 Swali la 15: Upimaji

Swali hili lilitoka katika mada ya Upimaji ambapo lililenga kupima uchambuzi. Mtahiniwa alitakiwa kufafanua faida sita za alama za majaribio katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3,140 ambapo, miongoni mwao watahiniwa 3,130 sawa na asilimia 99.7 walikuwa na ufaulu mzuri kwani walipata alama za wastani na za juu kuanzia 6 hadi 15. Chati Na.15 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 15:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 15*

Uchambuzi unaonesha kuwa swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyofanyika vizuri kutokana na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha na kuweza kufafanua faida sita za alama za majaribio katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa 2,942 sawa na asilimia 93.7 walifaulu vizuri na kupata alama kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hawa waliweza kupata alama za juu katika swali hili kwa sababu zifuatazo: baadhi ya watahiniwa waliweza kufafanua faida tano za alama za majaribio lakini walishindwa kufafanua faida mbili za alama za majaribio. Vile vile, watahiniwa wachache hawakuandika utangulizi na hitimisho katika majibu yao na watahiniwa wachache

waliweza kuandika faida za alama za majaribio na kuzifafanua faida hizo kwa kuzingatia matakwa ya swali hivyo walipata alama zote 15. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipata alama za juu baada ya kutoa faida zifuatazo za alama za majaribio katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji; *kukusanya takwimu za maendeleo ya darasani, kubaini na kubuni mbinu mbadala za ufundishaji, kufuatilia mienendo ya mwanafunzi mmoja mmoja na kuandaa mikakati ya ufundishaji.* Kielelezo Na.15.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu katika swali la 15.


15. Alama za majaribio ni jumla ya maksi zilizopatikana baada ya wanafunzi kufanya jaribio na mwalimu kukamilisha mchakato wa kusahihisha. Zifuatazo ni faida za alama za majaribio katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji:-

Humsaidia mwalimu kubaini maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma:- Alama za majaribio humsaidia au kumfanya mwalimu kujua iwapo mwanafunzi ameshuka au kupanda akilinganisha na alama za majaribio yaliyopita.

Humsaidia mwalimu kubaini matatizo ya wanafunzi katika kujifunza:- Kupitia alama za majaribio mbalimbali mwalimu huweza kujua matatizo mbalimbali ya wanafunzi wake katika ujifunzaji, kwa mfano anaweza kubaini wanafunzi ambao wanaelewa taratibu.

Huchochea ari ya ujifunzaji kwa wanafunzi:- Mwanafunzi kupitia alama za majaribio alizopata huweza kujitathimini na kuweka mikakati ya kuongeza alama katika majaribio mengine.

Husaidia kujua ni kwa kiasi gani malengo ya mtaala yamefikiwa; Wadau mbalimbali wa elimu huweza kujaribu kuangalia au kuchunguza ni kwa kiasi gani malengo ya mtaala yameweza kufikiwa kupitia alama mbalimbali za majaribio.

Humsaidia mwalimu kubuni mbinu na zana za kufundishia na →


15 Kujifunzia: Kwa kutumia alama za majaribio walizopata wanafunzi mwalimu huweza kumsaidia kubaini ~~mbinu~~ mapungufu ya mbinu na zana anazozitumia na hivyo kuchukua hatua za kufanya maboresho.
Husaidia kupanga wanafunzi katika mikondo: Baadhi ya shule hutumia alama za majaribio walizopata wanafunzi kama kigezo ambacho husaidia katika upangaji wa wanafunzi katika mikondo yaani wanafunzi huwekwa kwenye mikondo kulingana na alama zao za majaribio.
Kwa hiyo: Alama za majaribio zinazopatikana baada ya wanafunzi kufanya majaribio mbalimbali ni muhimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji

**Kielelzo Na.15.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 15

Katika kielelezo Na. 15.1 Mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi faida sita za alama za majaribio katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Vile vile, watahiniwa 10 sawa na asilimia 0.3 walipata ufaulu wa kiwango cha chini kwani walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5 kwa kuwa baadhi ya watahiniwa waliweza kutaja hoja zote lakini walishindwa kutetea hoja kulingana na matakwa ya swali. Kadhalika, watahiniwa wengine hawakuandika utangulizi wala hitimisho na baadhi ya hoja zao zilikuwa dhaifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile, *humsaidia mwalimu kubaini takwimu za maendeleo ya darasani, mwalimu huweza kubaini mbinu mbadala za ufundishaji, humsaidia mwalimu kufuatilia mienendo ya wanafunzi* lakini alishindwa kuzitolea maelezo sahihi. Pia, alitoa hoja ambazo hazikuwa sahihi kwa kuandika faida ya alama za uandishi kinyume na matakwa ya swali hivyo alipata alama za chini.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 188 sawa na asilimia 6 walipata alama hafifu kutokana na sababu kama vile: baadhi waliweza kutaja baadhi ya hoja kwa usahihi lakini walishindwa kuzitetea na hawakuwa na utangulizi wala hitimisho katika majibu yao. Watahiniwa wengine walitoa hoja ambazo

zilikuwa kinyume kabisa na matakwa ya swali hivyo walipata alama hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua kimakosa faida za alama za majaribio kama vile: *alama hutusaidia kukuza vipaji, husaidia kukuza akili, alama zinawezesha wazazi kutambua uwezo wa mtoto alama za uandishi hutumika kutolea zawadi kwa watahiniwa.* Kielelezo Na.15.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua faida sita za alama za majaribio katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.


15. Alama za Majaribio: Ni alama zote
zitumikazo kufanyiza majaribio mwanafunzi katika mchakato
kati mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Zifuatazo
faida mbalimbali zinazopatikana na alama za majaribio
faida hizi ni kama zifuatazo:
Alama hutusaidia kutuonyesha namna ya
utamkaji wa maneno kwa usahihi: kupitia alama
mbalimbali zitatuongoza na kutuonyesha msomaji namna
ya kutamka maneno katika lugha hatua kwa hatua
Alama za uandishi husaidia kukuza stadi ya
uandishi: kupitia alama mbalimbali za uandishi
mfano, nukta, mkato alama ya kuuliza huwawezesha
kukuza na kuwa uwezo wa kuandika kwa kila
mmoja kwa kuzingatia muelekezo ya alama husika
katika lugha au sentensi.
Alama zinatuwezesha wasomaji kutambua
malengo, maudhui na ujumbe unaopatikana kwa kila
alama: ujumbe huweza kufichua na alama mbali
mbali za maneno ya lugha hiyo, maudhui na




**Kielelezo Na.15.2:** Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Yasiyosahihi katika Swali la 15

Kielelezo Na. 15.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua matumizi ya alama za uandishi badala ya kufafanua faida za alama za majaribio.

### 2.3.3 Swali la 16: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya Ufundishaji ambapo lililenga kupima maarifa. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja sita kueleza jinsi atakavyofundisha nomino na vivumishi kwa wanafunzi wa darasa la sita.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 218 sawa na asilimia 6.7 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu. Watahiniwa 134 sawa na asilimia 61.5 walikuwa na ufaulu mzuri kwani walipata alama kuanzia 6 hadi 13 kama inavyoonekana katika Chati Na.16.




**Chati Na. 16**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 16*

Data za uchambuzi zinaonesha kuwa watahiniwa 111 sawa na asilimia 50.9 walijibu swali hili na walipata ufaulu wa wastani kwani walipata alama kuanzia 6 hadi 10. Hii ni kutokana na sababu zifuatazo: baadhi ya watahiniwa walitoa maelezo hafifu kuhusu nomino na vivumishi lakini pia hawakutoa maana ya nomino na kivumishi. Kadhalika, watahiniwa wengine walieleza kwa usahihi baadhi ya hoja na walishindwa kuelezea hoja zingine kutokana na kukosa maarifa juu ya namna ya kufundisha nomino na vivumishi kwa wanafunzi wa darasa la sita. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile; *kuwaongoza wanafunzi kutaja majina na vivumishi*, *kuandika ubaoni nomino na vivumishi* na *kuhitimisha kwa majadiliano kuhusu nomino na vivumishi* lakini alieleza hoja zingine kimakosa kwa kueleza aina za nomino kama vile*; nomino dhahania, nomino za pekee* na *nomino za jumla* hivyo alipata ufaulu wa wastani.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 84 sawa na asilimia 38.5 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5 kutokana na kukosa weledi juu ya jinsi ya kufundisha nomino na vivumishi kwa wanafunzi wa darasa la sita. Wengi wao, walishindwa kuelezea hoja nyingi na hawakuandika utangulizi wala hitimisho katika majibu yao.

Wachache walitoa majibu yaliyokuwa kinyume kabisa na matakwa ya swali. Aidha, majibu mengine ambayo hayakuwa sahihi yalikuwa katika kutoa maana ya nomino, kutoa tofauti iliyopo kati ya nomino na vivumishi, kutaja majina ya vitu na kuonesha vivumishi, kutoa vifupisho vya nomino na vivumishi na kutoa aina za nomino na vivumishi. Kielelezo Na.16.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutumia hoja sita kueleza jinsi atakavyofundisha nomino na vivumishi kwa wanafunzi wa darasa la sita.


16. Nomino ni aina ya majina yanayotaja vitu, watu, mahali katika mazingira mfano wa nomino kama Makongoro, Shule, Chuo, Ilonga hiyo ni mfano ya nomino. Vivumishi ni maneno yanayovumisha kitenzi katika sentensi vivumishi huweza kuvumisha maneno mbali mbali katika sentensi. Zifuatazo ni namna utakavyoweza kufundisha nomino na kivumishi kwa wanafunzi wa darasa la sita;
Vitu halisi; Hii ni njia ambayo mwalimu anaweza kuitumia katika kuwafundisha wanafunzi nomino kwa kutafsiri vitu halisi. Mfano katika nomino mwalimu anaweza kuchukua vitu halisi vyenye majina kufungamana na sehemu ilipo. Mfano darasani mwalimu anaweza kutumia vitu halisi kama madawati, ubao, chaki vivyohivyo hivyo katika vivumishi pia mwalimu anaweza kutumia;
Kwa kutumia Kamusi; Kamusi ni kitabu ambacho hutoa maana ya misamiati ya maneno hivyo kamusi inaweza kutumika katika mchakato wa kufundisha Nomino pamoja na kivumishi kwa kutafuta kufahamu aina za maneno na maana zake kwa ujumla
Majadiliano; Nomino pia huweza kufundishwa kwa njia ya kushirikisha wanafunzi katika vikundi hivyo mwalimu anaweza kuwagawa wanafunzi katika vikundi kwa kuzingatia usawa wa jinsia zao na kuwataka wajadili aina hizo za maneno ili kupata majibu au kuelezea mawazo yao na badae wakati wa uwasilishaji kila mtu au kila kundi liweze kuwasilisha kile walichokijadili na kutoa majibu




**Kielelezo Na. 16.1**: Majibu Yasiyosahihi katika Swali la 16

Kielelezo Na. 16.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyosahihi yaliyolenga kubaini vifaa na mbinu za kufundishia na kujifunzia badala ya kueleza jinsi ya kufundisha nomino na vivumishi kwa wanafunzi wa darasa la sita.

Watahiniwa waliopata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 13 katika swali hili walikuwa 23 sawa na asilimia 10.6. Uchambuzi unaonesha kuwa sababu za ufaulu huo ni pamoja na watahiniwa kukosa weledi juu ya mchakato mzima wa hatua za kufuata katika kufundisha aina za maneno hususan nomino na vivumishi katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya watahiniwa walijibu swali kwa ufasaha lakini hawakuandika utangulizi na hitimisho. Pamoja na hayo, watahiniwa wengine walitoa majibu sahihi lakini walishindwa kutetea ipasavyo

baadhi ya hoja. Pia, watahiniwa wachache walitoa hoja pungufu ingawa walizitetea kikamilifu. Kwa mfano, watahiniwa waliofanya vizuri katika swali hili walitoa majibu yafuatayo: *kuwafundisha kuhusu nomino na vivumishi* na *kuwasomea wanafunzi kifungu cha habari chenye nomino na vivumishi*, *kuwapa maswali ya mdomo ya kutaja nomino/vivumishi*, *kutumia chati ya michoro wenye baadhi ya nomino/vivumishi* na *kuwapa mazoezi ya kuandika kuhusu nomino/vivumishi*. Kielelezo Na.16.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali la 16.

15. Nomino ni maneno yanayotaja majina ya watu vitu au mahali na Vivumishi ni maneno yanayoelezea sifa za vitu. Zifuatazo ni namna/jinsi ya kuwafundisha nomino wanafunzi wa darasa la sita.

Kuwasomea kifungu cha habari ambacho kinaelezea maana na kutaja mifano ya baadhi ya nomino ndani yake; kupitia kusoma huku basi kutawafanya wanafunzi waweze kusikiliza kwa makini kifungungu hicho cha habari na hatimaye kupata maana na mifano ya nomino mbalimbali.

Kuwataka wanafunzi kutaja baadhi ya nomino wanazozifahamu kutokana kwa na kusikiliza kwao kile kifungu cha habari ambacho kimeeleza na kutaja mifano ya nomino.

Kutumia chati ya mchoro wenye baadhi ya nomino na kuwaongoza kusoma nomino hizo na kisha kuwataka wasome nomino hizo na ikiwezekana kila mmoja aweze kutaja nomino hizo.

Zifuatazo ni namna/jinsi ya kuwafundisha vivumishi wanafunzi wa darasa la sita.

Kuwasomea kifungu cha habari ambacho kinaelezea maana na kutaja mifano ya baadhi ya vivumishi ndani yake na kuwataka wasikilize kwa makini ili kupitia kusoma huko waweza kubaini maana ya vivumishi na kuweza kutaja baadhi ya vivumishi hivyo.

15. Kuwataka wanafunzi waweze kutaja baadhi ya vivumishi ambavyo wameweza kuvisikia kwenye kifungu cha habari na ikiwezekana waweze kutaja baazi ya sifa ambazo zinapatikana darasani kwa sababu vivumizi zinaelezea sifa kwa asilimia kubwa

Kutumia chati yenye mchoro ambayo imetaja baadhi ya vivumishi na kupitia chati hiyo utawaongoza kusoma kwa pamoja na baadye kila mmoja kwa nafasi yake kuweza kusoma pia.

Hivyo basi; Hizo ni njia ambazo zinaweza kutumika kuwafundisha nomino na vivumishi wanafunzi wa darasa la sita.

**Kielelezo Na. 16.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 16

Kielelezo Na. 16.2 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa yanayoeleza jinsi ya kufundisha nomino na vivumishi kwa wanafunzi wa darasa la sita.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa Ualimu wa Daraja A wa somo la Kiswahili ulikuwa na maswali (16) yaliyotoka katika mada 8. Mada hizo ni Utungaji, Upimaji katika somo la Kiswahili, Fasihi Simulizi, Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia somo la Kiswahili, Stadi za Lugha, Ufahamu, Sarufi na Zana za Kufundishia na Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Mada nne zilizokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu ni Sarufi, Ufahamu, Utungaji na Stadi za Lugha.

Uchambuzi wa kiwango cha ufaulu cha watahiniwa kwa mada unaonesha kuwa, watahiniwa wamefanya vizuri zaidi katika mada 4. Mada hizo ni Upimaji katika somo la Kiswahili (99.7%), Zana za Kufundishia na Ujifunzaji wa somo la Kiswahili (99.1%), Fasihi Simulizi (84.1%) na Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia somo la Kiswahili (74.3%) ambazo ni sawa na asilimia 50 ya mada zilizotahiniwa.

Kadhalika, unaonesha kuwa ufaulu ulikuwa wa kiwango cha wastani katika mada 4 ambazo ni Sarufi (69.6%), Ufahamu (65.6%), Utungaji (65.6) na Stadi za Lugha (54.3%).

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa wa miaka minne mfululizo toka mwaka 2018 hadi 2021 ni mzuri sana. Takwimu zinaonesha kuwa ufaulu katika miaka hiyo unapanda na kushuka kwani mwaka 2018 ufaulu ulikuwa (99.79%), mwaka 2019 (99.98%), mwaka 2020 (99.91%) na mwaka 2021 (99.94%). Hata hivyo, uchambuzi umedhihirisha wazi kwamba kiwango cha jumla cha ufaulu kwa mwaka 2021 kimepanda kwa asilimia 0.03 ukilinganisha na kile cha mwaka 2020.

## 4.0 HITIMISHO

Mtihani wa Ualimu wa Daraja A wa somo la Kiswahili kwa mwaka 2021 uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Kiswahili pamoja na Nyanja zake ambazo ni utambuzi, maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kiwango cha ufaulu kwa ujumla kilikuwa kizuri kwa kuwa asilimia 99.94 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa, ufaulu mzuri wa watahiniwa wa somo la Kiswahili ulitokana na sababu kama vile: kujibu kulingana na matakwa ya swali, uelewa mkubwa wa matakwa ya swali, maarifa ya mada kuu na mada ndogo, uwezo wa kutetea hoja walizotoa kwa kutumia mifano. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa waliweza kutoa hoja sahihi lakini wakashindwa kutoa mifano. Hivyo, kufanya kiwango cha ufaulu kuwa cha wastani.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ufaulu wa somo la Kiswahili ni mzuri kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2018. Ubora huu wa matokeo unatokana na jitihada mbalilmbali zinazofanywa na walimu tarajali, wakufunzi na serikali kwa ujumla. Ili kuendelea na ufaulu huu mzuri na hata kuboresha zaidi, wakufunzi wanashauriwa kufanya yafuatayo:

(a) Watumie mbinu ya midahalo, mijadala, makongamano na ziara za kimasomo kama mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji ambazo zitawaongezea walimu tarajali ujuzi na maarifa ili wawe na weledi katika mada za Sarufi, Ufahamu, Utungaji na Stadi za Lugha.

(b) Wawahimize walimu tarajali kutengeneza, kufaragua na kutumia zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili kwa kuzingatia mahitaji mbalimbali ya wanafunzi ili wajifunze kwa vitendo.

(c) Watumie mbinu ya matembezi ya galari ili kuhakikisha kila mwalimu tarajali anashiriki katika kujifunza mada mbalimbali kupitia katika makundi yaliyoandaliwa na wakufunzi.

(d) Watumie njia ya maswali na majibu, bungua bongo na vielelezo kuwaongoza walimu tarajali kuwa na weledi katika mada mbalimbali.

(e) Wahakikishe kuwa, mada zote zilizoainishwa katika muhtasari zinafundishwa kikamilifu na mbinu za kujifunzia zizingatie ushiriki wa walimu tarajali zaidi ili kuwawezesha walimu tarajali kuwa na umahiri katika mada zote jambo litakalowawezesha kuwa na ufaulu wa juu.

(f) Wawahimize walimu tarajali kuwa na ari ya kusoma vitabu na majarida mbalimbali ili kujijengea uwezo wa kutambua mada mbalimbali na kupata maarifa wakati wa ujifunzaji.

(g) Wawaandalie walimu tarajali mazoezi ya ufundishaji ya mara kwa mara ili kuwajengea umahiri wa kufundisha mada mbalimbali hususan mada za Sarufi, Ufahamu, Utungaji na Stadi za Lugha.

**Kiambatisho A**

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA 621 KISWAHILI

| Na | Mada | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Watahiniwa waliopata 40% ya alama au zaidi | Wastani | |
| 1 | Upimaji | 15 | 99.7 | 99.7 | Vizuri |
| 2 | Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili | 10 | 99 | 99.1 | Vizuri |
| | | 14 | 99.2 | | |
| 3 | Fasihi Simulizi | 1 | 76.4 | 84.1 | Vizuri |
| | | 5 | 80.4 | | |
| | | 11 | 95.4 | | |
| 4 | Mbinu za Kufundisha na Kujifunza Kiswahili | 6 | 94.4 | 76.3 | Vizuri |
| | | 8 | 58.2 | | |
| 5 | Sarufi | 3 | 77.6 | 69.6 | Wastani |
| | | 16 | 61.6 | | |
| 6 | Ufahamu | 4 | 63 | 65.6 | Wastani |
| | | 9 | 68.2 | | |
| 7 | Utungaji | 7 | 44.7 | 65.6 | Wastani |
| | | 13 | 86.5 | | |
| 8 | Stadi za Lugha | 2 | 13.9 | 54.3 | Wastani |
| | | 13 | 94.6 | | |

**Kiambatisho B**

## ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2020 NA 2021

